## Tunaamini Nini?

Kuona ni kuamini: maarifa na uzoefu zaidi utaleta matokeo bora katika kilimo. Kutakuwa ajira nyingi vijijini na wakulima wataongeza vipato vyao. Na kwa sababu ya kuboreshwa kwa uzalishaji wa mboga mboga, wenyeji wataweza kumudu gharama na kuongeza utumiaji wa mboga majumbani mwao. Hivyo SEVIA inachangia usalama na upatikanaji wa chakula, mapato zaidi kutokana na kilimo na afya njema.





The Sevia team




SEVIA

**Je, unahitaji habari zaidi? Tafadhali piga simu namba: +255 685 942 364**

SEVIA, S.L.P 7211, Moshi
Tutembelee: Lambo Mferejini, Hai
Barua pepe: info@sevia.biz
www.sevia.biz

MKULIMA WA

# SEVIA



# Seeing is believing

SEEDS OF EXPERTISE FOR THE VEGETABLE INDUSTRY OF AFRICA

## Kwa nani?

Kwa wakulima wa mboga mboga Tanzania.

## SEVIA ni nini?

Ni mradi unao onesha wakulima aina za mbegu zilizoboreshwa ili kuongeza ubora na wingi wa uzalishaji wa mboga mboga. SEVIA huonesha teknolojia bunifu na uzalishaji wa mazao kwa mbegu zilizoboreshwa.

## Jinsi gani?

Kwa kutumia mashamba darasa kwenye mashamba ya wakulima nchini; Kuona ni Kuamini. SEVIA inahusisha wataalamu wa sekta ya



kilimo cha mbogamboga wanaoelewa changamoto za wakulima. Mbali na hapo, tunatoa taarifa kuhusiana na mpango wa uzalishaji, taarifa za masoko, uchambuzi wa aina za mbegu, utunzaji wa kitalu, udhiti dhidi ya wadudu na magonjwa, matumizi bora ya maji, matumizi ya udongo na mbolea na shughuli nyingine.

## Na?

Mazao bora huzalishwa na aina za mbegu zilizoboreshwa na kwa usimamizi mzuri wa mazao. Na baada



ya kuvuna: Ni lazima kutunza mazao ilikusitiri ubora wake na kuongeza mauzo. SEVIA inaotoa elimu bora, itakayowezesha wakulima kufanikiwa.






## Tunafanya kazi wapi?

Mpaka sasa tuko ndani ya mikoa 10, nchini Tanzania. Mkoani Kilimanjaro, tuko wilaya ya Hai, tumeanzisha kituo cha utafiti na maonesho kwa shamba darasa, karibu na mji wa moshi, ambapo mbinu za kuboresha



kilimo cha mkulima mdogo hufanyiwa majaribisho na kuboreshwa. Maafisa ugani wa SEVIA huweka mashamba darasa kwa wakulima katika mikoa inayoongoza kwa kilimo cha mboga mboga nchini Tanzania ikiwemo: Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mwanza, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma na Pwani.

## Sisi ni nani?

SEVIA inaushirika na East- West Seed, Rijk Zwaan na Wageningen UR- Applied Plant Research Lelystad



na Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi. East West Seed na Rijk Zwaan ni makampuni yanayo ongoza duniani katika uboreshaji na uzalishaji wa mbegu. SEVIA inafanyakazi kwa ukaribu na Afrisem, program ya uzalishaji wa mbegu bora kwa ajili ya kuendeleza mboga mboga za Afrika. SEVIA inashirikiana na Tanzania Horticulture Association (TAHA), Chuo Kikuu cha Sokoine, AVRDC, HORTI-Tengeru na wataalam mbalimbali katika sekta hii nchini Tanzania. *Pamoja tunaweza!*